| Neno | Maana | Picha |
|---|---|---|
| **Maumivu kwenye maungio ya viungoviwili** | Tatizo la kiafya, ambapo sehemu za maungio ya mtu zinakuwa ngumu na kuvimbana/ au kuwa na maumivu wakati mtuanapojaribukuziinua. | |
| **Magurudumu yanayoweza kubadili mwelekeo** | Haya ni matairi ambayo hubadilisha muelekeo kila yanapotembea. Kwa mfano matari madogo yaliyo kwenye viti vya maofisini au sehemu ya mbele ya kiti cha magurudumu. | |
| **Katheta** | Mpira laini ambao unatumika kutoa mkojo kutoka kwenye kibofu cha mkono. Unatumiwa na watu ambao hawawezi kukojoa bila ya kupata msaada. Vifaa vingine vinaweza kuhitajika kulingana na aina ya katheta mfano begi ya mguuni. |  |
| **Vikwazo vya kimazingira** | Vikwazo katika mazingira ya mtu ( kwa mfano kuzunguka eneo analoishi, au kwenye jamii) ambavyo vinaweza kumzuia kuzunguka. Mfano vikwazo vya kimazingira ni:<br>• Ngazi zinazoleta ugumu kwa mtu anayetakakuzipanda kwa kutumia kiti cha magudurudumu manne.<br>• Njia ndogo ya kupita ambayo kwa mtu anayetumia fremu ya kutembelea hawezi kupita. | |
| **Udhaifu** | Hii ni kutokuwa na nguvu, kuumia kwaurahisi au kuwa na nguvu kidogo. Hutokea pale mtu anapokuwa kiumri na afya inapoanza kudorora | |
| **Chuma cha kushikiria** | Chuma kilicho kwenye ukuta ambacho mtu anaweza kushikilia ili kumsaidia kusogea. |  |
| **Kifaa cha kuinua** | Ni kifaa kinachomnyanyua mtu juu na kumsaidia kuhama kutoka sehemu moja kwenda nyingine. |  |
| **Kukosa uwezo wa kuruhusu nakuzuia haja ndogo/kubwa** | Pale mtu anapopata taabu au anaposhindwa kabisa kuruhusu na kuzuia h **Hoist** aja ndogo/kubwa. | |

| Neno | Maana | Picha |
|---|---|---|
| **Kifaasaidizi cha mkao** | Hiki ni nyongeza kwenye kiti cha magurudumu, kiti cha bafuni au msalani; vitu ambavyo vinampa mtu msaada. Vifaa saidizi vya mkao vinapaswa kugawiwa na mtu aliyepata mafunzo. Mifano wa Vifaa saidizi vya mkao kwenye kiti saidizi cha msalani na bafuni ni:<br>• Kamba yakujizungushia<br>• Uwepo wa msaada zaidi kutoka pembeni<br>• Sehemu ya kuegesha kichwa. |  |
| **Kidonda mgandamizo** | Kidonda mgandamizo kinatokana na kuharibika kwa ngozi Hii inatokea kwenye eneo lenye mfupa na inatokea mara nyingi kwa watu wenye matatizo ya hisia au wanaopata taabu kubadili mkao kutoka sehemu moja hadi nyingine | |
| **Jeraha kwenye Uti wa mgongo** | Mara nyingi uti wa mgongo unaumia kutokana na ajali au ugonjwa. Baada ya uti wa mgongo kuumia, jumbe zinakuwa haziwezi kusafiri vizuri kutoka sehemu nyingine ya mwili kwenda kwenye ubongo kupitia uti wa mgongo.. Kwa kawaida mtu hawezi kutembea (amepooza) na hawezi kuhisi maumivu kutoka kwenye eneo lililo chini ya eneo alililoumia. | |
| **Kiharusi** | Damu kutokufika vizuri kwenye ubongo. Hii inaweza kusababisha sehemu moja ya mwili kuwa dhaifu au kupooza na kusababisha matatizo mengine kama vile matatizo ya kuongea na kuhisi | |
| **Aina za vyoo:** | | |
| • **Choo cha kukalia** | Kiti ambacho watu hukalia ili kuweza kukitumia. |  |
| • **Choo cha kuchuchumaa** | Kiti ambacho watumiaji huchuchumaa juu yake ili kuweza kukitumia. |  |

| Neno | Maana | Picha |
|---|---|---|
| **Kuhama** | Kusogeza mwili kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine |  |